

SAUT

zetu

MULTILINGUAL

صداها • 声音 • أصوات • Amazwi • 聲 • 聲音 • Voices • Stammen • Sora • آوازين

Kiangazi 2024

www.houstonisd.org/voices

Toleo la III, Suala la 3

VIWANGO VYA UKUZAJI 2023-2024



Kwa wanafunzi wa HISD kukuzwa kwenye kiwango cha gredi inayofuata, lazima waoneshe kuwa wamefikia Viwango vya Ukuzaji vya HISD. Viwango hivi vinajumuisha gredi za darasa, uenyeji au majaribio ya nchi, na uhudhuriaji kama ifuatavyo:

- Mahitaji ya nchi ya jumla ya wastani wa gredi kila mwaka ya 70 au zaidi na mahitaji ya wenyeji wa gredi ya wastani wa 70 au juu katika sanaa ya lugha, hisabati, na sayansi na/ au masomo ya kijamii.
- Uhudhuriaji wa kutosha - jumla ya siku za kutohudhuria za mwanafunzi hazipaswi kupita asilimia 10 ya mikutano ya darasa.

[Viwango vya Ukuzaji 2023-2024](#)

[Estándares de promoción 2023-2024](#)

Kwa ujumbe zaidi kuhusu viwango vya ukuzaji kwa ziara za mwaka wa shule wa 2023-2024 [Mahitaji ya wanafunzi / Mahitaji ya Ukuzaji \(houstonisd.org\)](#)

UJUMBE WA SHULE YA KIANGAZI



Programu ya Kiangazi ya Ubakishaji wa Ukuzaji HISD kwa wanafunzi wa vidato PK-12 waliojisajili kufikia siku ya mwisho ya shule kwenye shule ya HISD na wanahitaji kufikia [viwango vya ukuzaji](#). Wakati unaoongezwa na programu za kiangazi unawapa wanafunzi nafasi nyongeza zilizojaa maelekezo makali na faafu na kutilia mkazo ili kufikia matarajio ya mwakani ya shule. Ni lengo la HISD kuwa kupitia programu faafu za kiangazi, wanafunzi wote wanaohitaji wakati huu wa ziada watafikia viwango vya ukuzaji vinavyohitajika, kuwa tayari kufuzu kwenye kiwango cha kidato kinachofuata, na kuwa kwenye mkondo wa kuhitimu na wenzao wa rika lao.

Tarehe muhimu za Shule ya Kiangazi

Jumatatu - Ijumaa

8 ASUBUHI - 2:45 ADHUHURI

Mwanzo: Jumatatu, Juni 17


Mwisho: Ijumaa, Julai 19

Likizo ya Shule ya Kiangazi (Hakuna Shule ya Kiangazi)
Juni 19, Julai 4, na Julai 5

Kwa ujumbe zaidi kuhusu shule ya kiangazi 2023-2024 zuru <https://www.houstonisd.org/summer>

MILO YA KIANGAZI

HISD itakuwa ikitoa kiamsha kinywa na chamcha kwa watoto wa umri 1-18 bure, Jumatatu hadi Alhamisi.



Lini: Juni 6 - Juni 30

Nyakati: inatofautiana kwa chuo

Mahali: Kupata pahali zuru <https://www.houstonisd.org/summer>

Kwa ujumbe zaidi kuhusu milo ya kiangazi zuru <https://www.houstonisd.org/Page/126922>



RASILIMALI ZA TEA

Kumsaidia Mtoto wangu

Rasilimali za kielimu za mtoto wako na mwelekezo wako



Misaada ya Familia

Rasilimali kwenye jamii yako kukusaidia wewe na familia yako



Rasilimali za Wanafunzi

Rasilimali za wanafunzi ambazo zinasaidia kujifunza kwako darasani



Tovuti ya English Learner-Ukurasa wa Nyumbani (txel.org)

Tovuti hii ya TEA imeundwa kukupa wewe na familia yako ujumbe na rasilimali kuhakikisha kufaulu kwa mtoto wako kiakademia.

Jiandikishe kama mteja kwenye tovuti ya TXEL kupokea rasilimali zenye msaada, sasisho, na ujumbe kuhusu hafla kuhusu jinsi ya kusaidia wanafunzi ibuka wa uwili-lugha.

Bonyeza hapa [kujandikisha](#).

Elimu ya Kujua Kusoma na Kuandika Nyumbani

Tunapoelekea mwisho wa mwaka wa shule na wazazi wanapoanza mipango ya kiangaazi, panga kujifunza kuhusu mchakato wa kujifunza kusoma au kujifunza lugha mpya. Rasilimali hapa chini zitakuelekeza kama mzazi kusaidia ujuzi wa kusoma na kuandika na maendeleo ya lugha ya mtoto wako. Hizi pamoja na rasilimali nyingine zilizoorodheshwa zitasaidia maendeleo ya lugha ya mwanafunzi wakati wa miezi ya kiangaazi.



ABCya

ABCya inatoa michezo inayofurahisha na ya kielimu zaidi ya 300 kwa vidato vya PreK hadi 6. Michezo imeainishwa kwa gredi na somo, na inaangazia mada kama vile kuzidisha, aina za maneno, kuandika, utambuzi wa mtindo, na zaidi.



Colorín Colorado

Ujumbe unapatikana kwa Kihispani

Vidokezo vya ujuzi wa kusoma na kuandika kwa wazazi wa wanafunzi wa miaka yote na orodha ya vitabu iliyopendekezwa kwa umri wa shule ya kati hadi ya upili.



Reading Rockets

Vidokezo kwa wazazi kuhusu kuhusika na njia za kusaidia usomaji wa mtoto wako.



Toolkit ya English Learner Family

Ujumbe wa familia kuhusu shule za umma Marekani.



Rasilimali za Kujifunza Uwili-lugha za Sesame Street

Ujumbe unapatikana kwa

Rasilimali za uwili-lugha kama mwelekeo wa shughuli za familia na video za watoto.

Kwa hizi na rasilimali nyingine zenye msaada zuru [English Learner Portal-Supporting My Child \(txel.org\)](#) na biringiza chini.

JARIDA LA TEA



Toleo hili la Parents and Families Newsletter linajumuisha ujumbe wa shughuli rahisi, za nyumbani kuongeza ushupavu wa mtoto wako na ujuzi kutumia michezo ya kielimu na shani za kujifunza, rasilimali zenye msaada, na mapendekezo kutoa msaada kwa mtoto wako.

Kituo cha Rasilimali

Tovuti za Wanafunzi za Kujifunza

Tovuti zifuatazo za kielimu ni rasilimali za bure ambazo zitasaidia mtoto wako kuboresha ujuzi wao wa lugha ya Kiingereza.



Jinsi vitu hufanyika?

[Jinsi Vitu Hufanyika](#)

[Soma Andika](#)
[Fikiria: Muumba](#)



[Toolkit ya Kuhlitemu ya TEA](#)

Kwa toleo la karibuni la Jarida la TEA zuru [Parents and Families Newsletter \(smore.com\)](#)

TAREHE MUHIMU ZA SCHOOL CHOICE

Kwa ujumbe zaidi zuru [HISD School Choice / Ukurasa wa Nyumbani \(houstonisd.org\)](#)

Ujumbe wa K-12	Tarehe
Tarehe ya mwisho ya Awamu ya Pili ya Kutuma Maombi	Agosti 2, 2024
Orodha ya kusubiri inataaifu	Agosti 9, 2024

Ujumbe wa Pre-K	Tarehe
Siku ya Kuarifiwa wazazi wa Pre-K Awamu ya 2 ya Pre-K inafunguliwa	Mei 10, 2024
Tarehe ya mwisho ya Awamu ya Pili ya Kutuma Maombi	Novemba 1, 2024
Orodha ya kusubiri inataaifu	Novemba 8, 2024

TAREHE MUHIMU ZA SCHOOL CHOICE



SUMMIT K12

Clever

Licha ya rasilimali zilizoorodheshwa hapa juu wanafunzi wa HISD wana ufikivu wa Summit K12 nyumbani kwa kuingia kwa Clever.

Summit K12 ni rasilimali kuu kwa wanaojifunza Kiingereza kuboresha ujuzi wa kusoma, kuandika, kusikiza, na kuzungumza. Mtaala nyongeza wa mtandaoni wenye vigezo vya viwango wa Summit K12 umethibitishwa kufunga nyufa kwa wanaojifunza Kiingereza na dakika 45- 60 tu za kazi kwa wiki.

Kuingia Clever zuru <https://clever.com/in/hisd/staff/portal>



Kufikia majarida yetu yote ya wazazi ya Programu za Multilingual bonyeza [hapa](#) au tambaza kodi ya QR.

Ikiwa una vidokezo vyovyote kuhusu mada ungetaka kusoma kuhusu, tafadhali tujulishe kwa kujaza huu [uchunguzi mfupi](#).

